# HALMASHAURI YA WILAYA YA KILWA

Shule ya Sekondari Kikole,
S.L.P 109,
**KILWA MASOKO.**

………./………/2020

***kikolesecondaryschool @yahoo.com***

**kumb.Na S2572/2021**
Jina la Mwanafunzi ………………………………
S.L.P …………………………

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KIKOLE WILAYA YA KILWA MKOA WA LINDI MWAKA 2021**

## 1.0 UTANGULIZI:

Nina furaha kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha I katika Shule hii mwaka 2021 Muhula wa kwanza utaanza tarehe 11/01/2021, unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 11/01/2021 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 01/02/2021

## 2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA:

2.1 Sare za Shule

(a) Sare za Shule hii ni sketi ndefu ya kijani kibichi zenye marinda ya kawaida kwa wasichana (ziwe 2) na suruali zisizo za kubana rangi ya kaki kwa wavulana (ziwe 2)
(b) Viatu vya rangi nyeusi vyenye kamba kwa wavulana na wasichana na soksi nyeupe. Pia mkanda mweusi kwa wavulana
(c) Rangi ya Hijab ni nyeupe ya mikono mirefu na shati jeupe la mikono mifupi kwa wavulana na wasiovaa hijab.
(d) Sare ya michezo kwa shule hii ni bukta bluu na fulana kwa wavulana na bukta ya nyekundu na fulana kwa wasichana.
(e) Anatakiwa awe na fulana yenye nembo ya shule itakayovaliwa siku ya jumatano na ijumaa na inapatikana shuleni kwa kulipia

2.2 Daftari 9 kubwa, kalamu za rangi ya bluu au nyeusi na mkebe wa hesabu.

2.3 Aje na vifaa vya kufanyia usafi shuleni, ufagio , kwanja (slashers) pamoja jembe lenye mpini

2.4 Mwanafunzi atakapofika kidato cha pili na nne itambidi kuhamia shuleni na gharama za chakula utalipa mzazi

2.5 Rimu 1(bunda la karatasi nyeupe) kwa ajili ya mitahani ya wiki na mwezi

## 3.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE:

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na.5 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na.10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote iliyotolewa na Wizara ya elimu na mafunzo ya ufundi yenye dhamana ya elimu nchini na ofisi ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapwa nakala yake.

(a) Kuheshimu kwa viongozi, wazazi, wafanya kazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
(c) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utazopewa.
(d) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka ya shule hiyo wakati wote wa uanafunzi wako wako katika shule hii.
(e) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
(f) Kuzingatia ratiba wakati wote.
(g) Kutunza mali za umma.

2.6 Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule

(a) Wizi
(b) Uasherati na ushoga
(c) Ubakaji
(d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji wa bangi, cocaine, mirungi, kuberi n.k
(e) Kupigana au kupiga
(f) Kuharibu kwa makusudi mali za umma
(g) Kudharau bendera ya Taifa
(h) Kuwa mjamzito/kupata mimba
(i) Kuoa na kuolewa
(j) Kutoa mimba
(k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
(l) Kukataa adhabu kwa makusudi
(m) Kuwa na simu ya mkononi shuleni

**4.0 Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi.**

(a) Medical examination form ambayo itajazwa na mganga mkuu wa Hospitali ya serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.
(b) Fomu ya maelekezo kuhusu historia ya mwafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
(c) Fomu ya mzazi kukiri kukabiliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

‘’***KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI KIKOLE***”

# UTHIBITISHO/KIAPO CHA MZAZI/MLEZI

Mimi.............................................................................................................. Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ............................................................................ Kidato cha ................... Mwaka ................ Nakubali asome katika shule ya sekondari kikole Ninathibitisha mwanafunzi huyu anaendelea vizuri kimasomo hivyo:-

A. Hana ruhusa ya kwenda kwenye nyumba za wageni, maeneo ya ulevi, kumbi za starehe, mataarabu n.k
B. Mimi mzazi/mlezi nitampatia vifaa vinavyohitajika hapa shuleni.
C. Ninaahidi kuwa nitahakikisha mtoto anafuata sheria na taratibu za shule. Hatua kali ichukuliwe dhidi yake kama atavunja taratibu na sheria za shule.
D. Ninaahidi kumleta shuleni mtoto wangu kwa wakati uliopangwa na uongoi shule bila kuchelewa. Kama atachelewa kuripoti shuleni nafasi yake ichukuliwe na mwanafunzi mwingine.
E. Anwani yangu ni:

.....................................................

.....................................................

.....................................................

.....................................................

Kazi ya mzazi/mlezi: Baba.........................................................................................
Mama.......................................................................................
Namba ya simu ya Baba..............................................................................................
Namba ya simu ya Mama ...........................................................................................
Saini ya Mzazi/Mlezi ............................................ Tarehe..........................................
Jina la Mwanafunzi............................................................................................ Saini ya Mwanafunzi ............................................... Tarehe .......................................

## CERTIFICATE OF MEDICAL EXAMINATION

The above named has been examined in respect of:-

(a) Stool ..............................................................................

(b) Urine ..............................................................................

(c) Chest ..............................................................................

(d) Blood ..............................................................................

(e) Eyes ..............................................................................

(f) Ears ..............................................................................

(g) Chronic Disease ......................................................

(h) Pregnancy Test (UPT) ................................................

(i) Others ..............................................................................

I have examined ........................................................................................... and consider his/her/fit/unfit to pursue as stated above.

........................................ ........................................

***Name of certifying Officer*** ***Signature***

........................................ ........................................

***Date*** ***Rubber Stamp*** ***Station***